HOTUBA YA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DR. MOHAMMED GHARIB BILAL, KWENYE MAADHIMISHO YA KITAIFA YA SIKU YA KUPIGA VITA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI, DAR ES SALAAM TAREHE 26 JUNI, 2011

Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Uratibu na Bunge),

Waheshimiwa Mawaziri,

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Waheshimiwa Wabunge,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Wastahiki Meya wa Manispaa za Jiji la Dar es Salaam,

Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa
Dawa za Kulevya,

Wakurugenzi wa Manispaa za Jiji la Dar es Salaam,

Viongozi mbalimbali,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Wananchi,
Awali ya yote naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na afya na tukaweza kuhudhuria katika maadhimisho haya muhimu. Pili napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa ya kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho haya ya kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani. Pia, nawapongeza viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja ana Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa kujiandaa na kufanikisha maadhimisho haya. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru ninyi wananchi mliojitokeza na kujumuika hapa uwanjani kwa wingi kuadhimisha siku hii muhimu. Ahsanteni sana kwa kufika na kufanikisha maadhimisho haya.

Ndugu Wananchi,
Tatizo la biashara haramu ya dawa za kulevya na matumizi yake duniani ni kubwa na linazidi kuongezeka siku hadi siku. Tanzania kama zilivyo nchi zingine duniani imekumbwa na tatizo hili kwa kiasi kikubwa na linaathiri sana maendeleo ya taifa letu. Hali imekuwa mbaya zaidi ambapo baadhi ya Watanzania wanajihusisha na biashara hii haramu hadi nje ya mipaka ya nchi yetu. Kwa mfano, katika kipindi cha 2005 hadi 2010 Watanzania 211 walikamatwa nje ya nchi kwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Baadhi yao

wamehukumiwa kunyongwa na wengine wanatumikia vifungo katika nchi mbalimbali kama China, India, Pakistan na Iran. Hali hii inashusha hadhi ya nchi yetu katika mahusiano ya kimataifa.

Ndugu Wananchi,
Leo taifa letu linaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hii muhimu kwa lengo la kukumbushana wajibu wetu katika kupambana na janga hili. Kauli Mbiu ya maadhimisho haya ni **"MIAKA 50 YA UHURU" TANZANIA HURU BILA DAWA ZA KULEVYA INAWEZEKANA"** Ujumbe huu unahimiza Watanzania kuongeza nguvu za udhibiti wa dawa za kulevya hasa katika kipindi hiki ambacho tunajiandaa kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru. Uhuru wetu utakuwa na maana iwapo tutaongeza juhudi katika kulitokomeza janga hili na hatimaye kuifanya jamii ya Mtanzania kuishi bila kufanya biashara wala kutumia dawa haramu za kulevya.

Ndugu Wananchi,
Hapo awali, tatizo la dawa za kulevya lilikuwa dogo na lilihusisha zaidi bangi na mirungi, na kwa wakati huo aina nyingine za dawa za kulevya zilikua zikipitishwa tu hapa nchini kuelekea sehemu nyingine duniani. Kwa sasa hali imebadilika, utumiaji wa dawa za kulevya za viwandani hasa heroin, Cocaine na Mandrax, umeongezeka kwa kasi na nchi yetu imegeuzwa kuwa soko la dawa hizo. Aidha, ukubwa wa mipaka ya nchi yetu, mabadiliko ya kukua kwa uchumi na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, kumesababisha dawa za kulevya kuingizwa kwa urahisi hapa nchini pamoja na juhudi kubwa ya kuzizuia.

Ndugu Wananchi,
Idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya inazidi kuongezeka na maeneo yenye tatizo hili hapa nchini pia yameongezeka. Kwa sasa watumiaji wanapatikana maendeo yote si mjini tu bali hata vijijini na cha kusikitisha zaidi ni kwamba matumizi hayo sasa yameanza kujitokeza miongoni mwa watoto waliopo mashuleni na mitaani. Watoto wetu wako katika hatari kubwa sana ya kuangukia kwenye janga hili, hii ni kutokana na ukweli kwamba hawana uwezo wa kujilinda bali wanahitaji ulinzi kutoka kwetu sisi wazazi na walezi wao. Watoto hawana uwezo mkubwa wala ujuzi wa kujua njia na namna ya kukabiliana na janga la dawa za kulevya, na mara nyingi wamekuwa wakirubuniwa na kujikuta kwenye matumizi ya dawa hizo hatari. Natoa wito kwa shule na asasi zinazohusika na malezi ya watoto na wanafunzi kuhakikisha kuwa watoto katika maeneo yao wanabaki salama na kuepuka matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Hivyo basi, ni wajibu wa kila kiongozi wa Serikali, dini, mzazi, mlezi, mwalimu kuhakikisha watoto wadogo wanalelewa katika maadili mema, na mazingira ya elimu yanakuwa huru bila dawa za kulevya.

Ninapenda kusisitiza kuwa janga hili halina ulinzi mbadala kwa watoto wetu, isipokuwa wazazi na walezi tu, ambao wanatakiwa kuwa karibu sana na watoto

wao. Tusiache watoto walelewe na Televisheni na Intaneti kwani mitandao hii ina taarifa nyingi ambazo hazifai kwa watoto wetu.

Ndugu Wananchi,
Biashara na matumizi ya dawa za kulevya vina madhara mengi kiuchumi, kiafya na kijamii. Biashara ya dawa za kulevya huvuruga uchumi wa nchi kwa njia mbalimbali zikiwemo kusababisha mfumuko wa bei kutokana na mzunguko wa fedha haramu. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya hudhoofisha afya za watumiaji na kuathiri uwezo wao wa kufanya kazi. Halikadhalika, dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo ya ini, mapafu, moyo, kifua kikuu na akili ambapo jamii yetu imekuwa ikishuhudia kuongezeka kwa wagonjwa wa akili mitaani kunakosababishwa na matumizi ya dawa hizo.

Ndugu Wananchi,
Matumizi ya dawa za kulevya, huchochea maambukizi ya VVU hasa kwa wanaotumia dawa hizo kwa njia ya kujidunga sindano au kufanya ngono zisizo salama. Madhara mengine ni pamoja na kuongezeka kwa ajali za barabarani, kumomonyoka kwa maadili katika jamii, uhalifu kama vile ujambazi, wizi na ubakaji. Biashara haramu ya dawa za kulevya huambatana na rushwa na wakati mwingine mauaji.

Ndugu Wananchi,
Kutokana na madhara yanayosababishwa na biashara haramu ya dawa za kulevya, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali zenye lengo la kulinusuru Taifa kutokana na janga hili. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, kama vile, radio, televisheni na magazeti. Njia nyingine ni kwa kutumia mabango, machapisho na ushiriki katika matukio maalum ya kitaifa na kimataifa kama ilivyo kwa siku hii. Aidha, mafunzo kwa watendaji wanaojihusisha na udhibiti wa dawa za kulenya yamekuwa yakitolewa ikiwa ni pamoja na asasi za kiraia na vikundi vya kijamii. Halikadhalika, Serikali iko katika mchakato wa kuandaa chombo mahsusi huru na chenye nguvu cha kupambana na dawa za kulevya. Ni matumaini yetu kuwa chombo hicho kikishaundwa kitaongeza jitihada za serikali katika kupambana na janga hili.

Ndugu Wananchi,
Serikali imekuwa ikitoa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya katika hospitali mbalimbali hapa nchini. Ili kuongeza utoaji wa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya, serikali inajenga kituo maalum cha kisasa cha tiba Mkoani Dodoma kitakachosaidia kuondoa tatizo la kuwachanganya wagonjwa wa afya ya akili na watumiaji wa dawa za kulevya. Kituo hicho pia kitatoa mafunzo kwa watendaji wa tiba na utengemano.

Natoa wito kwa waathirika wa dawa za kulevya kujitokeza kwa wingi katika vituo vya afya kupata matibabu. Aidha, waathirika wa dawa za kulevya wasinyanyapaliwe na jamii inayowazunguka bali wasaidiwe kwa kufikishwa katika vituo vya ushauri na tiba. Pia, tuongeze nguvu katika kutoa elimu dhidi ya athari za dawa za kulevya na kuweka msisitizo katika kuwahudumia watumiaji ili waachane na matumizi ya dawa hizo.

Ndugu Wananchi,
Serikali inajitahidi kudhibiti tatizo la dawa za kulevya kwa kukamata dawa za kulevya pamoja na wafanyabiashara wa dawa hizo haramu. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 mpaka 2010 jumla ya watuhumiwa 30,830 walikamatwa kwa makosa mbalimbali ya biashara ya dawa za kulevya na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Bangi imeendelea kuwa tatizo kubwa kwa vile inastawi katika maeneo mengi ya nchi yetu. Kutokana na kushamiri kwa kilimo hicho, jitihada zimeelekezwa katika uteketezaji wa mashamba ya bangi. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010 jumla ya ekeri 2,166 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika baadhi ya mikoa hapa nchini.

Ndugu Wananchi,
Serikali imepata mafanikio makubwa katika kupambana na janga la biashara na matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kushirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo mashirika mbalimbali yasiyokuwa ya kiserikali ya ndani na nje ya nchi pamoja na vikundi vya kijamii. Hivyo nachukua fursa hii kuvipongeza vyombo vya dola pamoja na wadau wote kwa kazi nzuri na jitihada kubwa katika kukabiliana na tatizo hili. Aidha, Serikali inatambua na kuthamini kazi ngumu mnazozifanya katika mapambano haya na tunaahidi kuendelea kushirikiana nanyi katika kukabiliana na tatizo hili. Vilevile, natoa wito kwa mashirika na asasi zinazojihusisha na masuala ya watoto, elimu, kuondoa umaskini, vita dhidi ya UKIMWI na mengineyo wajihusishe pia na suala la kupambana na matumizi na biashara ya dawa haramu za kulevya kwani ni suala mtambuka. Mikakati ya aina mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hili imeendelea na itaendelea kubuniwa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Ndugu Wananchi,
Vita dhidi ya biashara ya dawa za kulevya si rahisi, ni ngumu sana kutokana na ukweli kwamba katika mapambano haya tunashindana na watu hatari sana, wajanja na wenye mitandao ikiwemo ya kimataifa. Kutokana na hali hiyo, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinahitaji ushirikiano kutoka kwa kila mmoja wetu.

Hivyo basi, naagiza kila mwananchi mwenye mapenzi mema na nchi yetu atoe taarifa kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama pale anapobaini kuwepo kwa watu wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya. Ningepandekeza

pia kwamba suala la madawa ya kulevya na athari zake liingizwe katika mitaala ya shule zetu za Msingi na Sekondari.

Ndugu Wananchi,
Nimalizie kwa kuwakumbusha kwamba janga la biashara na matumizi ya dawa za kulevya ni letu sote, humgusa kila mtu kwa namna moja au nyingine na lina athari kubwa sana, hivyo tunapaswa kushirikiana katika kukabiliana na changamoto za mapambano dhidi ya dawa za kulevya. **"MIAKA 50 YA UHURU" TANZANIA HURU BILA DAWA ZA KULEVYA INAWEZEKANA"** Nchi yetu imethubutu, imeweza na inasonga mbele katika kupambana na dawa za kulevya.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.